

HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA

SHULE YA SEKONDARI KINING'INILA,
S.L.P 206,
IGUNGA.

08/12/2020.

KUMB Na KSS/FJ.39/01

Mzazi/Mlezi wa:.....

S.L.P

IGUNGA.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KINING'INILA WILAYA YA IGUNGA MKOA WA TABORA MWAKA 2021

1.0 Utangulizi

Ninafurahi kukanififi kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari Kining'inila, ipo umbali wa Km 43 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Igunga. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021, unatakiwa kuripoti shulenii tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 25/01/2021 ndani ya siku kumi na nne (14). Baada ya hapo wazazi/mlezi wataripotiwa katika mamlaka husika kwa kosa la kutowahudhurisha wanafunzi shulenii.

2.0 Mambo muhimu ya Kuzingatia

2.1 Sare za Shule

(a). WASICHANA

- (i). Sketi mbili (2) za rangi ya kijivu zenyenye Linda box nje isiwea yenxye "V" na urefu uzidi magoti kwenda chini.
- (ii). Shati mbili(2) nyeupe (tetroni) mikono mifupi zenyenye nembo ya shule.
- (iii). Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na visigino virefu wala urembo na vyenye kamba (jozi 2)
- (iv). Soksi ndefu nyeupe.
- (v). Viatu vya michezo (raba nyeusi) jozi moja.
- (vi). Hijabu inaruhusiwa iwe ya heshima na ifanane na sare za shule
- (vii). Sweta rangi ya kijivu
- (viii). T-Shirt rangi ya njano yenye nembo ya shule kwa ajili ya michezo na shughuli za nje.
- (ix). Wanafunzi hawaruhusiwi kusuka nywele.

(b). WAVULANA

- (i). Suruali za kijivu zenyenye mifuko miwili pembedi na mmoja wa nyuma na ziwe na marinda mawili tu.
- (ii). Shati mbili nyeupe (tetroni) mikono mifupi zenyenye nembo ya shule na tai
- (iii). Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na visigino wala urembo (jozi 2) vyenye kamba.
- (iv). Soksi nyeusi
- (v). Viatu vya michezo/raba nyeupe (jozi moja)
- (vi). Sweta rangi ya kijivu
- (vii). T – shirt rangi ya njano yenye nembo ya shule.

2.2 Mahitaji muhimu kwa wanafunzi

- (i).Daftari kubwa 12 (Counter book 2Q)
- (ii).Kalamu (bluu au nyeusi) 10
- (iii).Mathematics sets 1 (Mkebe wa hesabu)
- (iv).Pnseli 2
- (v).Rula 1
- (vi).Faili (Plastic file)
- (vii).Ufagio wa kufagia nje (chelewa) 1
- (viii).Fyekeo

KARIBU SANA KINING'INILA SEKONDARI

.....
JOHN S. KANILIZU
MKUU WA SHULE

3.0 SHERIA ZA SHULE NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaongozwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenyes dhamana ya Elimu chini ya Ofisi ya Rais TAMISEMI yenyecu jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo pamoja na kanuni na taratibu za shule ziliwekwa kwa mujibu wa sheria. Hivyo unatakiwa kuwa na:-

3.1 SHERIA ZA SHULE

Ni marufuku mwanafunzi kufanya yafuatayo:-

- (i). Kutoka nje ya shule kabla ya mda wa kuruhusiwa bila kibali.
- (ii). Kuzurula nje wakati wa vipindi.
- (iii). Kuwa na simu shuleni.
- (iv). Kufuga ndevu, nywele, kucha, kupaka rangi na kusuka nywele.
- (v). Kuingia bila ruhusa sehemu zifuatazo;.Ofisi za walimu,maabara,jikoni,Hosteli na nyumba za wafanyakazi.
- (vi). Kutembelea vilabu vya pombe , kumbi za starehe kwenye sehemu za kucheza kamali na nyumba za kulala wageni.
- (vii). Kukimbia mitihani na majaribio.

3.2 MWANAFUNZI ATAFUKUZWA SHULE KAMA ATAFANYA

MAKOSA YAFUATAYO:-

- (i). Kusababisha au kupata mimba.
- (ii). Kupiga au kupigana
- (iii). Kutoroka shuleni
- (iv). Kugoma kufanya adhabu AU Kumpiga mwalimu
- (v). Kujihusisha na wizi
- (vi). Kukutwa na simu shuleni
- (vii). Kuhamasisha migomo.
- (viii). Kushiriki matendo ya uhalifu.
- (ix). Kujihusisha na mapenzi ndani na nje ya shule.
- (x). Kutumia kilevi cha aina yoyote.
- (xi). Kudharau wimbo au bendera ya taifa.
- (xii). Kuoa au kuolewa
- (xiii). Uasherati na ushoga

3.3 SEHEMU ZILIZOKATAZWA

- (i). Kuingia nyumba za kulala wageni (Guest House)
- (ii). Kumbi za starehe
- (iii). Sehemu za kuuzia pombe
- (iv). Nyumba za walimu
- (v). Maabara isipokuwa wakati wa kipindi au kibali maalumu.

4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KWASILISHWA SHULENI NA WANAFUNZI

- (i). Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitli ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
- (ii). Fomu ya maelekezo binafs kuhusu historia ya Mwanafnz na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- (iii). Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatayotolewa na shule.

5.0 Tafadhal soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.